TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MAADHIMISHO YA SHEREHE ZA WAKULIMA TAREHE 01 -08 AGOSTI, 2008

Ndugu Wananchi,

Awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kuwakaribisha wakulima, wafugaji na wadau wote kwenye maadhimisho ya Nane Nane ya mwaka 2008 ambayo ni ya 15 tangu kuanzishwa kwake. Lengo la Sikukuu hii ni kuwatambua na kuwaenzi wadau wakuu wa sekta ya kilimo ambao ni wakulima, wafugaji, wanaushirika, wasindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na maliasili kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu. Lengo ni kuhakikisha sherehe za Nane Nane zinaadhimishwa nchi nzima kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa, Kanda na Taifa.

Ndugu Wananchi,

Mwaka huu wa 2008, sherehe hizi zinafanyika Kitaifa mjini Dodoma katika Uwanja wa Maonyesho ya Kilimo wa Nzuguni uliopo kilomita saba kandokando mwa barabara ya Dar es Salaam kwenda Dodoma. Nashukuru na kuupongeza uongozi wa mikoa ya Dodoma na Singida pamoja na *Tanzania Agricultural Society (TASO)* kwa juhudi zao za kufanikisha kuingiza uwanjani huduma za msingi ambazo ni maji na umeme. Changamoto kubwa iliyopo mbele yetu sote ni kuendeleza uwanja huu kwa kujenga mabanda ya maonyesho, kuandaa vipando na kuboresha huduma ili zikidhi mahitaji ya maonyesho hayo Kikanda na Kitaifa.

Uwanja wa Nzuguni ni wa nne katika mchakato wa kuandaa viwanja vya Kanda vya maonyesho ya Kilimo. Lengo la Serikali ni kuiwezesha kila kanda ya kilimo nchini kuwa na uwanja wa maonyesho ya Kilimo ambao utakuwa na hadhi ya kuandaa maonyesho kwa ajili ya kuwaelimisha wadau wa sekta ya Kilimo wakati wa sherehe za Nane Nane na nyakati zingine za mwaka kulingana na mazingira yao. Hadi sasa, Serikali kwa kushirikiana na TASO imefanikiwa kuwa na viwanja vya maonyesho ya wakulima katika kanda zifuatazo:

- Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Tanga) – uwanja wa Maonyesho ya Kilimo wa Mwl. J.K. Nyerere, upo eneo la Tungi, Morogoro;

- Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma) – Uwanja wa Maonyesho ya Kilimo wa John Mwakangale, upo eneo la Uyole, Mbeya;

- Kanda ya Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro na Manyara) – Uwanja wa Maonyesho ya Kilimo wa Themi, upo eneo la Njiro, Arusha.

Ndugu Wananchi,

Wakati wa sherehe hizi za Nane Nane, Wakulima, Wafugaji, Wanaushirika na wadau wengine katika sekta za Kilimo, hupata fursa nzuri zaidi ya kuona na kujifunza mbinu na teknolojia sahihi za uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo, maliasili na bidhaa nyinginezo kupitia Maonyesho ya Kilimo yanayoandaliwa. Aidha, kwa wafanyabiashara huwa ni fursa nzuri ya kutangaza bidhaa zao hususan pembejeo na zana mbalimbali za uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na maliasili.

Sherehe hizi za Nane Nane husimamiwa na TASO na washiriki wakuu ni Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Taasisi za Serikali, Taasisi zisizo za Serikali (NGOs), Makampuni ya umma na binafsi, Vyama vya Ushirika, Wafanyabiashara, Vikundi vya Wakulima, Wafugaji na Watu binafsi.

Ndugu Wananchi,

Kaulimbiu ya sherehe za Nane Nane Mwaka huu ni "**Mapinduzi ya Kijani Ndiyo Mkombozi wa Mtanzania".** Kaulimbiu hii imechaguliwa baada ya kutafakari kwa undani suala zima la ***Umaskini*** na nafasi ya ***Kilimo cha mazao, ufugaji, ushirika na hifadhi ya mazingira*** zinavyoweza kuchangia katika harakati za kutokomeza umaskini. Sekta hizi kwa pamoja, zikiendelezwa ipasavyo zinaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kuondoa umaskini na upungufu wa chakula nchini.

Kaulimbiu ya mwaka huu inahimiza wakulima, wafugaji na wanaushirika kuleta mapinduzi katika Kilimo na ufugaji kwa kuzingatia mbinu na kanuni bora za Kilimo na ufugaji.

Ndugu Wananchi,

Inafahamika kwamba wakulima na wafugaji hufarijika sana na kutiwa moyo kwa ushiriki wa dhati wa viongozi wa ngazi zote kuanzia ngazi ya Taifa hadi vijijini katika maandalizi na katika sherehe za Nane Nane mara zote zinapofanyika nchini. Hivyo, kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita, mwaka huu pia viongozi wa Ki-Taifa na ngazi nyingine wataendelea kushirikiana nasi katika maadhimisho ya mwaka huu kuanzia siku ya uzinduzi utakaofanyika tarehe 01 Agosti, 2008 hadi siku ya kilele cha sherehe hizo tarehe 08 Agosti, 2008.

Kama ilivyo ada, maonyesho ya mwaka huu yanazingatia kuwaonyesha wananchi mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya Kilimo, ufugaji na ushirika pamoja na kuwaonyesha na kuwafundisha mbinu bora za Kilimo. Aidha, kutokana na changamoto za upungufu wa upatikanaji wa chakula duniani na katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu, maonyesho ya mwaka huu yatajikita katika kuwafahamisha wananchi juu ya umuhimu wa kuzalisha kwa tija zaidi kwa kutumia teknolojia bora. Lengo ni kuwajengea uwezo wakulima na wafugaji kupambana na hali ya umaskini ili wapate maisha bora.

Ndugu Wananchi,

Kwa taarifa hii napenda kutoa wito kwa wadau wote wa sekta za Kilimo, Ufugaji, Ushirika na Mazingira pamoja na wananchi wote kushiriki kwa dhati katika maonyesho ya mwaka huu. Napenda kusisitiza kwamba mahudhurio yenu katika maonyesho hayo yatakuwa ya manufaa makubwa kwani mtajionea mbinu za kuboresha shughuli zenu za kilimo, ufugaji, ushirika na masoko ya mazao yenu. Kwa wale wanunuzi na upande wa wafanyabiashara watapata fursa ya kutangaza bidhaa zao. Tunawakaribisha nyote tushirikiane pamoja kufanikisha sherehe hizi za Nane Nane kwa mwaka wa 2008.

Natoa wito kwa wadau wote kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya sherehe hizo na kuhudhuria kwa wingi maonyesho hayo kutoka tarehe 1 Agosti hadi 8 Agosti, 2008.

Ahsanteni kwa kunisikiliza,

Stephen M. Wasira (Mb)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA